



MAAFA ya DATSI

Je Daniel alikuwa jasiri vya kutosha kusema ukweli?

Na Kimberly Oldroyd
(Imetokana na hadithi ya kweli)

Hadithi hii ilitokea huko Marekani.

Daniel alitoa mfuniko wa zamani wa sanduku la mwanasesere la Babu yake na kuchungulia ndani. Binamu zake walikusanyika kuangalia. Walipenda kucheza pamoja nyumbani kwa Babu!

Ndani yake mlikuwa na wanasesere wengi ambao mama na shangazi wa Daniel waliwachezea walipokuwa watoto.

“Hizo ni nini?” Binamu wa Daniel, Noah, alionyesha kwenye datu sita zinazong’aa za mtindo wa kizamani. Zilikuwa na miisho yenye kuchongoka na bendera zenye rangi—baadhi nyekundu na baadhi njano.

Daniel alinyanyua mojawapo. “Mama yangu aliniambia kuhusu hizi,” alisema. “Unatengeneza duara kwenye nyasi. Kisha mnachukuwa zamu kuzirusha hewani na kujaribu kuzifanya ziangukie ndani ya duara.”

“Safi sana!” alisema Noah. Alikuwa tayari akikimbia kuelekea kwenye uwanja kuutayarisha mchezo.

Mara Daniel na binamu zake walikuwa wakirusha datu za chuma angani kuzunguka uwanja mzima wa Babu. Daniel alipenda wakati datu zilipotua kwa kishindo na kukwama katika nyasi.

“Nakuhakikishia naweza kutupa zangu juu zaidi kuliko zako,” alisema binamu wa Daniel aitwaye Lily.

Watoto walicheka na walirusha datu juu na juu.

Kisha Daniel akawa na wazo. “Nakuhakikishia naweza kurusha zangu kwenye njia nzima mpaka itumbukie ndani ya duara!” alisema. Alikimbilia upande mwingine wa njia na alirusha datu kwa nguvu sana.

Datu iliruka juu hewani, lakini haikutua ndani ya nyasi. Badala yake ilianguka kwenye gari jipya kabisa la shangazi Robilyn kwa sauti kubwa ya **KISHINDO**.

“Oh hapana!” Noah alipiga kelele.

Daniel alichukua datu ile. Kulikuwa na mbonyeo mkubwa mno kwenye gari pale ilipoanguka.

Watoto walitazamana kwa kuogopa sana. Kisha, bila kusema chochote, waliziacha datu kwenye uwanja na wakakimbilia ndani.

Baadaye mchana ule, kila mmoja aliingia kwenye magari yao kwenda nyumbani. Shangazi wa Daniel aligundua mbonyeo kwenye gari lake. “Kilitokea nini?” aliuliza.

Tumbo la Daniel likahisi kuwa zito. Lakini hakusema chochote. Aliingia tu kwenye gari na akapunga kwaheri kwa binamu zake.

Wakiwa njiani kurejea nyumbani, Daniel alikaa kimya kwenye kiti cha nyuma. Alijaribu kusoma kitabu chake. Lakini hakuweza kufokasi. Alijihisi vibaya ndani kuhusu kile kilichotokea. Alijua kuwa mwaminifu kulikuwa kitu sahihi cha kufanya. Lakini kusema ukweli kutakuwa ni kitu cha kutisha! Wazazi wake watakuwa wakali mno juu yake. Na ndivyo itakavyokuwa kwa shangazi yake.

Kisha Daniel alikumbuka kuhusu shujaa wake mpendwa wa maandiko. Daniel katika Agano la Kale alitupwa ndani ya tundu la simba kwa ajili ya kuchagua kilicho sahihi. Alikuwa jasiri. Inawezekana Daniel angeweza kuwa shujaa pia.


“Mama?” Daniel alisema. “Nilitupa datu uwanjani na ilipiga gari la Shangazi Robilyn na kutengeneza mbonyeo. Ilikuwa ni kosa langu,”

Mama alimtaazama katika kioo cha kuangalia nyuma. Hakuwa na hasira kali kama Daniel alivyofikiri angekuwa. “Asante kwa kuniambia ukweli,” alisema.

Daniel alivuta pumzi mzito. “Naweza kumwita Shangazi Robilyn tutakapofika nyumbani?” Daniel aliuliza. “Ninataka kusema samahani. Na nitafanya kazi kwa nguvu kupata fedha ya kulipia na kutengeneza gari lake.”

Mama alitabasamu. “Hilo ni wazo zuri sana.”

Hisia nzito tumboni mwake ilikuwa haipo tena, na Daniel alihisi amani. Amekuwa jasiri vya kutosha kueleza ukweli. Kwa sababu ya Yesu Kristo, aliweza kutubu na kufanya mambo kuwa sawa. ●



Ni kwa jinsi gani Daniel alihisi wakati alipoeleza ukweli na kutubu?

VIELELEZO NA JOSH TALBOT